

## Ndoa

Tukisoma mwanzo wa uumbaji katika Mwanzo 1-3, tunaona Mungu aliumba mwanamke moja kwa ajili ya mwanaume. Ni mpango wa Mungu kila mwanaume awe na msaidizi wake na msaidizi wake awe mwanamke. Mungu hakuumba wanawake wawili au zaidi kwa Adamu bali moja tu na ndivyo inavyotaka leo. Bila kujali tunataka nini, Mungu aliumba mwanamke kwa mwanaume, siyo wanawake kwa mwanaume!

### I. Ndoa Ilianzishwa Na Mungu:

- A. Mwa. 2:18, Mungu hakutaka mwanaume aishi peke \_\_\_\_\_.
- B. Mwa. 2:18-22, Mungu aliumba mwanamke awe \_\_\_\_\_.
- C. Mwa. 2:23-24; Mat. 19:5-6, ndoa ya kwanza ilianzishwa na \_\_\_\_\_.
- D. Malaki 2:14, \_\_\_\_\_ ni shahidi wa \_\_\_\_\_.
- E. Ebr. 13:4, Ndoa iheshimiwe na \_\_\_\_\_.
- F. 1 Kor. 7:1-5, Ni njia ya kuzuia zinaa.
- G. 1 Kor. 7:7-9, Ni njia ya kuzuia tamaa mbaya.
- H. Mat. 19:6, \_\_\_\_\_ na Mungu, mwanadamu \_\_\_\_\_.

### II. Dhambi Katika Ndoa:

- A. Kuwa na wanawake zaidi ya mke moja:
  - 1. Mwa. 1:27, 28; 2:22-23, Hapo mwanzo Mungu alimpa Adamu mke \_\_\_\_\_.
  - 2. Mwa. 2:24; Mat. 19:4-5, Na mwanaume pamoja na mwanamke wakawa \_\_\_\_\_.
  - 3. Mwa. 4:19, Kuoa wanawake wengi kulianzishwa na ukoo mbovu wa \_\_\_\_\_.
  - 4. Ingawaje baadhi ya wanaume wa Agano La Kale walikuwa na wake wengi, walipata tabu sana kwa kufanya hivyo:
    - a. Ibrahimu - Mwa. 16:4-6; 21:9-10.
    - b. Daudi - 2 Sam. 13:1-38; 2 Sam. 15:18.
    - c. Sulemani - 1 Fal. 11:1-8.

Taja matatizo walikuwa nayo Ibrahimu, Daudi na Sulemani kwa sababu walioa wengi.

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_.

- 5. Yesu Kristo alikataa tabia hii ya kuoa wake wengi, Mat. 19:4-5.
- 6. Roho Mtakatifu alifundisha kwamba kila mwanaume anapaswa kuwa na mke, 1 Kor. 7:1-3.
- 7. Mtu yeyote atakayeo au kuolewa na mwingine anazini, Rum. 7:2-3; Gal. 5:19-21.

## B. Kutengana Au Talaka:

1. Tunaweza kuoa au kuolewa kwa watu gani?
  - a. 1 Kor. 7:9, \_\_\_\_\_.
  - b. Wale ambao walio au waliolewa lakini mwezako akifariki, Rum. 7:2-3.
  - c. Wale walioachana na mwenzake kwa sababu ya uasherati, Mt. 19:9 (Lakini hatuna uwezo kuoa au kuolewa kwa yule alioachwa kwa sababu ya uasherati).

### Hitimisho:

Tukumbuke ndoa ilianzishwa na Mungu, na ni lazima tufuate maneno yake kama tunataka Mungu atubarikie ndoa zetu. Na kama Mungu atakataa kubariki ndoa zetu kwa sababu ya uasherati au mitala ni lazima tuache dhambi kama tunataka kurithi ufalme wa mbinguni.